

kampuni zimejiunga kuunga mkono hata kwa kuchangia maji ya kunywa na mambo mengine," alisema.

Alipoulizwa kuhusu bajeti iliyotengwa kukamilisha shughuli hiyo, Mkunda alisema: "Suala la bajeti lipo chini ya kamati siwezi kusema ni bajeti kiasi gani, ambacho naweza

Chanzo cha kazi mwema... hifadhi ya jina gazetini, kilidai migogoro inayotokea ndani ya vyama imechangia kudhoofisha shughuli zinazofanywa na TUCTA za kukusanya michango kutoka vyama mbalimbali kati ya 18 vinavyounda Shirikisho. "Kukosekana kwa mshikamano na

kwamba... ya msingi. "Ni kweli mishahara haijaongezwa kwa muda mrefu, binafsi natamani sana kuona kwa mwaka huu mishahara ya watumishi inaongezeka," alisema Rais Samia.

Rais Mwinyi kwa kuendeleza na kukuzwa uchumi wa Zanzibar, hasa katika sera ya uchumi wa buluu ambayo aliahidi kwenda kuifanyia kazi Malawi.

# \* Sera yaboresha ufugaji, pato la Taifa \*

Na Lucas Raphael, Tabora

**K**UWAPO Sera ya Taifa ya Mifugo nchini kumechochea kwa kiasi kikubwa uboreshaji sekta ya mifugo na kuwezesha pato la Taifa kuongezeka kutoka Sh trilioni moja mwaka 2006/07 hadi Sh trilioni 10.6 mwaka 2020/21.

Hayo yalibainishwa juzi na Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora. Msalika Makungu kwenye kikao cha mapitio ya utekelezaji sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006, kilichohudhuriwa na wadau wakiwamo wakuu wa idara za mifugo wa mikoa ya

Dodoma, Singida, Tabora na Katavi na kufanyika kwenye ukumbi wa Mtemi Isike Mwanakinyugi.

Alisema sera hiyo iliyoidhinishwa na kuanza kutumika nchini mwaka 2006 licha ya changamoto kadhaa, imekuwa na tija kubwa kwa ukuaji wa sekta hiyo, ikiwamo kutoa fursa kwa wadau wa mifugo kufanya shughuli zao.

Alibainisha mafanikio yaliyopatikana kupitia sera hiyo, kuwa ni kuongezeka kwa mchango wa sekta ya mifugo kwenye pato la Taifa, kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya mwaka 2021 ambapo pato la Taifa lilikuwa Sh trilioni 148.5.

Faida nyingine ni ongezeko la mifugo kutoka ng'ombe milioni 18.5 hadi milioni 33.9, mbuzi kutoka milioni 13.1 hadi milioni 24.5, kondoo kutoka milioni 3.5 hadi milioni 8.5 na kuku kutoka milioni 30 hadi milioni 87.7.

Aidha idadi ya viwanda vya kusindika maziwa vimeongezeka kutoka 22 mwaka 2005/06 hadi 105 mwaka 2020/21, machinjio za kisasa kutoka mbili hadi 24, maabara 12 za kuchunguza magonjwa ya mifugo zilianzishwa na minada kuboreshwa.

Msalika aliongeza kuwa katika kipindi cha

miaka 15 ya uwepo wa sera hiyo, uwekezaji kwenye viwanda vya nyama umeongezeka kutoka kiwanda kimoja hadi 11. majesho kutoka 1,860 hadi 2,763 na kujengwa kiwanda cha kuzalisha chanjo za mifugo ambacho sasa kinazalisha chanjo saba badala ya tano za awali.

"Mafanikio haya yamechangia kuimua maisha ya wananchi kiuchumi, kuchangia upatikanaji malighafi katika viwanda vya kuchakata na kusindika mazao ya mifugo, kuinua biashara za mazao ya mifugo na nje ya nchi na kuboresha lishe katika kazi," alisema.